



Jinsi ya kuchanja soya: kwa kutumia Legume Fix



1

Pima kilo 15 za mbegu ya soya na ziweke katika ndoo au beseni la lita 20. Kiasi hiki cha mbegu kinatosha kupanda eneo la nusu eka.



2

Pima vijiko 14 vya chai au gramu 75 za chanjo, kisha weka katika mbegu zilizo pimwa.



3

Changanya mbegu na chanjo na hakikisha chanjo imechanganyika na kushikamana vyema na mbegu.



4

Mbegu tayari zimechanjwa, zifunike kwa kutumia kitambaa safi, karatasi au kiroba ili kuzikinga dhidi ya miale ya jua na ziweke kivulini tayari kwa kupanda.

FAIDA ZA CHANJO:

- Chanjo uhakikisha mmea utoaji wa vinundu (nodules) vingi.
- Utoaji mzuri wa vinundu husaidia mimea jamii ya mikunde kujitengenezea nitrojeni.
- Nitrogeni inapotengenezwa kwa wingi, mavuno huongezeka, na mazao yanayopandwa baada ya mavuno au yanayopandwa mseto na mimea jamii ya mikunde hufaidika pia na nitrojeni iliyotengenezwa.
- Matumizi ya chanjo yana unafuu katika gharama kuliko matumizi mbolea za nitrogen kutoka viwandani.

Zingatia:

- Gramu 100 za chanjo zinatoa kuchanja kilo 25 za mbegu. Kwa kiwango kidogo cha mbegu, tumia kijiko kimoja cha chai au kizibo cha chupa ya soda (chenye uzito wa gramu 5) cha chanjo kwa kila kilo moja ya mbegu.
- Chanjo sahihi itumike kwa mbegu sahihi, usitumie chanjo ya maharagwe kuchanja mbegu ya soya.
- Chanjo huambatana na viumbe hai (bacteria rafiki) vinavyo hitaji kulingwa dhidi ya miale ya jua. Hakikisha unahifadhi chanjo katika mazingira yenye hali ya ubaridi na dhidi ya miale ya jua mfano kwenye chungu cha udongo au maeneo yenye ubaridi ndani ya nyumba.
- Chanjo hupoteza nguvu inapohifadhiwa sehemu ya wazi. Daima hifadhi chanjo kwenye pakiti yake na itumike mara tu inapofunguliwa.
- Mbegu zichanjwe muda mfupi kabla ya kupanda.
- Chanjo isitumike baada ya muda wake wa matumizi kupita.

Kufanya kazi kwa pamoja na wadau/wabia kutayarisha taarifa zinazohusu mbinu husishi za afya ya udongo